

FURSA HAIJI MARA MBILI: Jinsi unavyoweza kupata faida au hasara ukitumia Nafasi au fursa uliyonayo

By SW - Melkisedeck Shine · January 10, 2016

Biashara - Mbinu za Ujasiriamali na Biashara Kufanya tofauti · #Karibu AckySHINE · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF · #Ujasiriamali: Fursa za Maendeleo na Biashara · #Ujasiriamali: Kujitambua na Kuwa na Mafanikio Katika Maisha

Kwenye maisha fursa moja tu inatosha kabisa kubadilisha hali yako ya sasa na kukuweka kwenye kiwango kingine kabisa cha mafanikio. Kuna watu wengi sana ambao waliwahi kufikiria kuwa maisha yao yatachukua miaka mingi sana kabla hayajabadilika na kwa mshangao wao walipoanza kufanya vitu sahihi wakakutana na mabadiliko makubwa sana katika maisha yao kwa kupitia fursa moja tu.

Kufanikiwa kwenye maisha ni matokeo ya kujua mambo sahihi ya kuyafanya. Ni kama ilivyo wakati unapotaka kufungua mlango uliofungwa, unachohitaji ni ufunguo sahihi wa kutumia na sio vinginevyo. Ili ufanikiwe lazima uwe mtu mwenye bidii na ambaye unawathamini watu bila kujali hali zao za sasa. Ili kutoka hapo ulipo na kwenda kule unakotaka unahitaji watu wa kukuunganisha na fursa mpya, kukuonyesha njia nzuri ya kufanya mambo, wa kukurekebisha na watu ambao unaweza kujifunza kwao.